

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

UPUNGUFU KATIKA KUTIMIZA VIWANGO BORA VYA UZALISHAJI DAWA (GMP) ULIOONEKANA KATIKA VIWANDA VYA RANBAXY VILIVYOKO DEWAS NA PAONTA SAHIB NCHINI INDIA

Kama ambavyo imeripotiwa kwenye vyombo vya habari, Mamlaka ya Udhhibiti wa Chakula na Dawa ya Marekani (US Food and Drug Administration) mnamo tarehe 16 Septemba 2008 ilitoa barua mbili za onyo kwa kiwanda cha Ranbaxy Laboratories Ltd cha India na pia kutoa tahadhari kuhusu uingizaji wa dawa kutoka katika sehemu mbili ambapo dawa za Ranbaxy zinatengenezwa au kutumia malighafi zinazozalishwa na viwanda hivyo kwa sababu ya upungufu ulioonekana katika kukidhi viwango bora vya uzalishaji dawa (Good Manufacturing Practice). Maana ya uamuzi huu ni kwamba Maafisa wa Serikali ya Marekani wanaweza kuzuia dawa na malighafi zinazozalishwa na viwanda hivi viwili katika mipaka ya nchi hiyo.

Jumatano ya tarehe 17 Septemba 2008, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitoa taarifa kuhusiana na suala hili na kuelezea hatua inazozichukua kukabiliana na hali hii ikiwa ni pamoja na kuwaomba walaji kuendelea kutumia dawa za viwanda hivi wakati likiendelea kuchukua hatua za ziada ili kuhakikisha kwamba Ranbaxy inaendelea kuchukua hatua muhimu za kurekebisha hali hii.

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) imesajili dawa kutoka katika viwanda hivi viwili na dawa hizi ziko katika soko. TFDA inapenda kuufahamisha umma kwamba suala hili linafuatiliwa kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuchukua sampuli za dawa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kama kuna matatizo ya ubora ambayo yanaweza kufanya dawa hizo zisiwe salama.

Aidha, TFDA inawashauri wagonjwa kuendelea kutumia dawa zao na pale ambapo watakuwa na wasi wasi wawasiliane na madaktari wao au TFDA.

Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
S.L.P. 77150, Dar es salaam
Simu: +255-22-2450512/2450751/2452108
Faksi: +255-22-2450793
Barua Pepe: info@tfda.or.tz Tovuti: www.tfd.or.tz